# Kiswahili kama Kichocheo cha Maendeleo ya Kiuchumi katika Nchi za Afrika Mashariki

*James O. Ontieri*
*Chuo Kikuu cha Maasai Mara, Kenya*

**Ikisiri**

**Kiswahili ni lugha ya matumizi mapana katika ukanda wa Afrika Mashariki. Katika juhudi ya kujiendeleza kiuchumi, jamii mbalimbali zinahitaji lugha ya mawasiliano ambayo inaeleweka kwa wahusika kama njia kuu ya kuafikia maendeleo. Aidha, kunahitajika juhudi za kimakusudi miongoni mwa wananchi za kuimarisha viwango vyao katika matumizi ya Kiswahili ili kuitumia lugha hiyo katika kushirikisha mipango anuwai ya kimaendeleo katika nyanja za kiuchumi. Ni kutokana na hali hii ambapo makala haya yanaonyesha mchango wa Kiswahili katika suala zima la maendeleo ya kiuchumi katika nchi za Afrika Mashariki. Data ya makala haya ilikusanywa kupitia kwa upekuzi wa maandishi yanayohusu mchango wa lugha katika maendeleo ya jamii pamoja na yale yanayohusu hali halisi ya maendeleo ya kiuchumi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.**

**Maneno Muhimu**: Kiswahili, Kichocheo, Maendeleo, Kiuchumi, Afrika Mashariki.

## Utangulizi

Lugha ni chombo muhimu katika juhudi za kufanikisha mawasiliano miongoni mwa wanajamii. Shughuli zote katika jamii hutegemea lugha inayoeleweka kwa wahusika. Anavyoeleza Nwadike (2004), lugha ndiyo ufunguo wa kufungulia mioyo ya wanadamu. Anaendelea kusema kwamba tukiuthamini huu ufunguo basi itakuwa rahisi kuleta maendeleo ya kitaifa. Masuala ya uchumi wa nchi na maendeleo mbalimbali yatawezekana tu ikiwa lugha ya matumizi mapana itakuzwa ili kuwasaidia wanajamii wakati wanaposhughulikia mikakati anuwai ya kujiendeleza katika nyanja husika. Ni bayana kuwa bila kuwapo kwa lugha ya aina hiyo hakutakuwa na maendeleo katika eneo husika. Katika eneo zima la Afrika Mashariki Kiswahili ndiyo lugha ya matumizi mapana kutokana na kueleweka kwake kwa wanajamii wengi wanaoishi katika maeneo mbalimbali. Matumizi haya mapana yana mchango mkubwa katika kuimarika kwa uchumi wa nchi za eneo hili. Kwa mujibu wa Mukuthuria (2006), hapana shaka kuwa hivi leo Kiswahili ni kati ya lugha kuu za kienyeji katika bara la Afrika ambazo

zinachangia maendeleo. Anaendelea kueleza kuwa zile nchi ambazo zimekubali kuiendeleza lugha hii kama vile Tanzania na Kenya, ziko mbele kuliko zile nyingine ambazo hazijajitahidi kuikuza lugha hii. Mukuthuria (mtaje) anasisitiza kwamba eneo zima la Afrika Mashariki na kati huitumia lugha hii kuimarisha biashara, usomaji na umoja. Hatua ya hivi majuzi ya Rwanda kukifanya Kiswahili lugha rasmi inastahili kupongezwa na jumuiya nzima ya Afrika Mashariki kwa kuwa inachangia katika kuweka msingi imara wa wananchi kunufaika hususan wanapowasiliana na wenzao katika eneo hili. Kwa jumla nchi za Afrika Mashariki zinapojitahidi kukuza matumizi ya Kiswahili kwa mapana, ni wazi kuwa zitapata manufaa mengi kutokana na ustawi utakaoshuhudiwa katika nyanja tofauti hasa ile ya kiuchumi.

Juhudi za kuimarisha uchumi zinatakiwa kuchangiwa na umma katika nchi husika. Hili litawezekana pale ambapo tabaka la watawala katika jamii litagundua kuwa lugha za kienyeji ndizo vyombo muhimu vya kuwasilisha ujumbe kwa raia. Kulingana na Prah (1993), mtanziko barani Afrika unasababishwa na mazoea ya tabaka aali la wenye uwezo ambalo limenaswa na utamaduni wa jamii za kimagharibi. Wao huiona Afrika kwa mtazamo wa kimagharibi huku wakithamini lugha za kizungu na kudunisha zile za kiafrika. Hivyo basi, utaratibu wowote unaolenga kuleta maendeleo ya kiuchumi, shuruti uelekezwe na ukweli kwamba lugha za kienyeji ndizo msingi wa ustawi wa aina hiyo. Aidha, ni muhimu ikumbukwe kuwa, maendeleo ya jamii hayatokani na watu wachache ambao wametwikwa jukumu la uongozi bali umma ambao huelewa na kutumia lugha za kienyeji. Ibainike kuwa lugha za kikoloni, zile za viongozi na wenye uwezo, zina mchango mdogo sana katika uimarishaji wa uchumi. Hizi lugha hutumiwa wakati wa kuendesha biashara na nchi za kigeni ambazo hazitumii Kiswahili katika mawasiliano. Hali hii pia hujitokeza katika shughuli za kitalii hasa nchi zetu zinapopokea watalii kutoka nchi za kigeni kama vile Ulaya, Marekani na Asia. Lugha za kiafrika kama vile Kiswahili zinachangia pakubwa katika kuupalilia na kuundeleza uchumi wa mataifa mbalimbali hasa katika eneo la Afrika Mashariki.

Makala haya yanashughulikia matumizi ya Kiswahili katika eneo la Afrika mashariki kwa kulenga mchango wake katika ustawi wa kiuchumi. Kati ya vipengele vikuu tunavyovishughulikia ni pamoja na: Kiswahili kama lugha ya matumizi mapana; Kiswahili na ustawi wa biashara; Kiswahili na uzalishaji bidhaa viwandani na Kiswahili katika sekta za kutoa huduma. Masuala haya yanachunguzwa kwa kuweka wazi nafasi ya Kiswahili katika kuendeleza hali ya uchumi wa eneo zima.

## Kiswahili kama Lugha ya Matumizi Mapana

Tunapozungumzia lugha ya matumizi mapana tuna maana ya lugha inayotumiwa na watu kutoka jamii-lugha tofauti kwa lengo la kurahisisha mawasiliano kati

yao. Kwa mujibu wa TUKI (2009) hii ni lugha ya biashara/ mawasiliano kama vile Kiswahili katika eneo la lugha nyingi mbalimbali. Ikumbukwe kwamba lugha ya Kiingereza imekuwa lugha ya matumizi mapana katika sehemu mbalimbali za ulimwengu kwa muda mrefu. Imekuwa ikikidhi haja ya mawasiliano miongoni mwa watu wanaozungumza lugha tofauti za kienyeji.

Kiswahili kinaeleweka na wengi na wa matabaka mbalimbali katika jamii za Afrika Mashariki na Kati. Mukuthuria (2006) anaeleza kuwa nchi za Afrika Mashariki zinafanya juhudi za kimakusudi kuweka misingi ya kuwa na sera ya lugha moja inayotumiwa katika eneo zima. Hali hii inatarajiwa kuwezesha upitishaji wa habari baina ya nchi husika kuwa rahisi na hata kuongeza idadi ya watu wanaovuka mpaka ili kuendeleza shughuli za kiuchumi katika sehemu mbalimbali. Ni kutokana na haja hii ambapo kipengele cha 19 (b) cha mkataba wa kuundwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kinasisitiza umuhimu wa kustawisha na kuendeleza lugha za kienyeji hasa Kiswahili kama lugha ya matumizi mapana katika eneo hili.

Akisisitiza kuhusu nafasi ya Kiswahili kama lingua franka ya Afrika Mashariki na Kati, Kitula (1999), anasema kuwa lugha hii ilitumika kama msimbo wa kupitishia elimu katika vipindi mbalimbali vya kihistoria. Anaendelea kueleza kwamba kutokana na uchache wa watu wanaozungumza Kiingereza (20%), lugha ya Kiswahili ina nafasi muhimu kama chombo cha mawasiliano ya kijamii na maendeleo. Kauli hii inatusisitizia umuhimu wa Kiswahili kama lugha iliyo na jukumu la kuwezesha wananchi kushiriki katika shughuli za kiuchumi. Ili kutimiza malengo ya ukuaji wa uchumi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, shuruti umma ushirikishwe kikamilifu. Njia kuu ya kuushirikisha umma, ni kupitia kwa matumizi ya lugha inayoeleweka barabara. Utaratibu kuhusu mikakati inayopaswa kuzingatiwa ili kustawisha uchumi, unastahili kuwasilishwa kwa lugha ya Kiswahili ambayo hutumiwa na idadi kubwa ya wananchi katika eneo zima la jumuiya katika mawasiliano yao ya kila siku - katika maeneo ambamo watu wa jamii-lugha tofauti huishi. Tunapochunguza matumizi ya lugha katika maeneo mengi ya vijijini, tunaona kwamba lugha ya Kiswahili hueleweka na hata kutumiwa na wananchi katika mawasiliano kuliko Kiingereza ambayo huchukuliwa kama lugha ya walioelimika. Ni bayana kwamba, itakuwa rahisi kumshawishi mtu afanye utakalo kwa kutumia lugha anayoilewa kuliko ile asiyoielewa. Masuala ya kiuchumi yataeleweka na kutekelezwa kwa urahisi na wananchi ikiwa yatawasilishwa kwa lugha inayoeleweka hususani Kiswahili katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Sehemu nyingi za ulimwengu zimegundua umuhimu wa kustawisha lugha mahsusi kwa ajili ya matumizi mapana. Matokeo ya hali hii ni ustawi wa wanajamii mbalimbali katika nyanja anuwai kama vile kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kuhusu uimarikaji wa kiuchumi, nchi mbalimbali hutegemea uhusika wa

wanajamii katika shughuli tofauti za kuzalisha mali. Maeneo kama vile Ulaya na Marekani hutegemea lugha zinazoeleweka na watu wengi kama vile Kiingereza katika kuratibu na kuimarisha shughuli za kiuchumi. Hali hii inadhihirika kupitia kwa miungano kama Muungano wa Ulaya unaolenga kuendeleza uchumi wa nchi husika. Lugha za matumizi mapana hutumika katika mazingira kama haya ili wahusika kuelewana wanaposhughulikia uwekezaji na biashara kwa jumla.

**Kiswahili na Ustawi wa Biashara**

Lugha ni mtikati wa mawasiliano katika jamii yoyote ile. Ni kupitia kwa mawasiliano ambapo binadamu huwa na uwezo wa kuendesha shughuli mbalimbali katika jamii. Mwingiliano wa kibiashara utawezekana kukiwa na lugha ya mawasiliano inayoeleweka kwa pande mbili zinazohusika. Lugha ya Kiswahili ina umuhimu wa kipekee katika kutimiza haja ya kimawasiliano katika eneo la Afrika Mashariki na hivyo kuendeleza shughuli za kibiashara zinazolenga kuimarisha uchumi wa nchi husika. Akishadidia umuhimu wa lugha katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo, Djite (2009) anasema kuwa bila lugha hakuwezi kuwa na maendeleo na katika bara la Afrika maendeleo kamili yatafikiwa ikiwa kutakuwa na utangamano wa rasilimali watu. Anaeleza kuwa maendeleo huathiriwa na uteuzi ya lugha itakayotumiwa katika jamii husika. Matumizi ya Kiswahili yanaweza kudhihirika katika shughuli mbili kuu: Mawasiliano kati ya wafanyibiashara na matangazo ya biashara. Shughuli hizi zinajadiliwa katika sehemu inayofuata.

**Mawasiliano kati ya Wafanyibiashara**

Kihistoria lugha ya Kiswahili imekuwa ikitumiwa kama chombo cha mawasiliano katika sehemu mbalimbali za Afrika Mashariki kwa miaka mingi. Kulingana na Chiraghdin na Mnyampala (1977), Kiswahili kilitumiwa wa wafanyibiashara walioingia bara kutafuta bidhaa anuwai. Misafara ya biashara iliyoanzia pwani kuingia bara ilifanikiwa katika malengo yake ya kuendeleza biashara kwa kuwa wahusika walikuwa wanaelewa lugha ya Kiswahili na waliitumia ili kupitisha ujumbe kwa jamii iliyokuwa na bidhaa muhimu. Kila msafara ulihitaji watu mamia hadi maelfu wa kubeba mizigo ya biashara kutoka pwani hadi pale msafara ulipolenga hata Ziwa Tanganyika. Watu hawa wote walisambaza matumizi ya Kiswahili katika sehemu za ndani.

Kiswahili kama lugha ya matumizi mapana ina nafasi muhimu katika mawasiliano kati ya jamii-lugha mbalimbali katika eneo la Afrika Mashariki. Kutokana na idadi kubwa ya watu wanaoishi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (zaidi ya milioni 150), inamaanisha kuwa soko la bidhaa mbalimbali ni kubwa na linahitaji ushirikishi ili kuleta manufaa ya kiuchumi. Kuwapo kwa Kiswahili kama lugha inayoeleweka na watu wengi mijini na vijijini katika eneo hili kunatoa nafasi ya kipekee kwa ustawi wa biashara katika nchi mbalimbali na baina ya nchi za Afrika Mashariki. Ikumbukwe kuwa enzi za wafanyibiashara

kubadilishana bidhaa bila kuongea zimepita na wala hatuzitarajii kurudi. Kwa sasa shughuli zote za kibiashara zinaendelezwa kwa kutumia lugha inayoeleweka na pande zote husika. Kupitia kwa matumizi ya Kiswahili katika uendeshaji wa biashara, ni bayana kuwa tutaondoa ufinyu wa soko kwa kuwa kutakuwa na uwezekano wa wafanyibiashara katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kuuza bidhaa zao popote bila kufungika katika nchi zao. Ni muhimu kuelewa kwamba lugha ina nafasi muhimu katika kuimarisha uchumi tukichukulia mfano wa Uchina ambayo imestawi mno kiuchumi kwa kutumia lugha yao kuwafikia wateja wao katika sehemu mbalimbali za nchi hiyo. Bidhaa mbalimbali zinazozalishwa kule Uchina huwafikia wakazi wa nchi hiyo bila tatizo lolote kwa kuwa wana lugha ya Kichina inayowaunganisha wananchi wote.

Hali inayoshuhudiwa katika masoko mbalimbali ni kwamba mazungumzo hutawala shughuli nzima. Wahusika kwa mfano hutaka kupunguziwa bei kabla ya kununua bidhaa zinazouzwa. Inasisitizwa kwamba kila lugha duniani huambatana na utamaduni fulani wa watumiaji wake. Waswahili wamekuwa na mazoea ya kutumia Kiswahili kwa biashara kwa namna ambayo muuzaji hutaja bei ya juu kidogo kisha mnunuzi huomba punguzo mpaka pale ile bei itakapowaridhisha wote wawili. Mwandishi wa BBC Arnold Kayanda alitembelea Soko Kuu la Kariakoo jijini Dar es Salaam ambako alisikiliza mtizamo wa Waswahili kukosa nafasi hiyo ya 'nipunguzie kidogo' kutoka kwa wafanyibiashara wa Kichina (www.bbc.com). Hivyo basi, ni muhimu kwa muuzaji na mnunuaji kutumia lugha kama chombo cha kuwasilisha mawazo yao kuhusu bei inayofaa kabla ya kukubaliana na kukamilisha shughuli hiyo. Ni wazi kwamba ikiwa hakutakuwa na lugha ya kuwaleta pamoja wahusika, biashara hiyo haitaendeshwa vizuri na hivyo kupelekea kudumaa kwa ukuaji wa kiuchumi. Kiswahili kitakuwa muhimu sana katika mazingira kama haya hususani ikiwa wafanyibiashara wanaielewa lugha hii na kuitumia kikamilifu katika juhudi za kuendeleza biashara yao. Hali ya mawasiliano kwa lugha inayoeleweka kwa muuzaji na mnunuzi huchangia pakubwa katika kufanikisha biashara na hivyo kupelekea kuimarika kwa uchumi wa eneo husika. Hivyo basi, ni wazi kuwa kutokana na juhudi za kimakusudi za viongozi wa kisiasa kuhimiza matumizi ya Kiswahili katika eneo la Afrika Mashariki, biashara inatarajiwa kuimarika kwa kiasi kikubwa.

### Kiswahili na Matangazo ya Biashara

Matangazo ya biashara ni mtikati katika juhudi za kufanikisha biashara na hivyo kuinua uchumi wa nchi au eneo. Huu ni mchakato ambao huleta habari kuhusu bidhaa fulani na mahali zinakopatikana kwa wateja. Ili makampuni na mashirika ya kibiashara kufanikiwa katika juhudi hizi, matumizi ya lugha ya matumizi mapana ina umuhimu mkubwa. Tunapochukua mfano wa vyombo vya habari kama vile redio, runinga na magazeti, tunagundua kwamba wawezekaji wengi hutumia vyombo hivi katika kutangaza bidhaa na huduma zao. Ili kuifikia hadhira

pana na hivyo kupata faida kubwa kutokana na mauzo husika, matangazo huwasilishwa kwa lugha inayoeleweka kwa wateja wengi. Ni bayana kuwa Kiswahili ndiyo lugha inayoeleweka na hata kutumiwa na watu wengi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sasa. Hali hii inaifanya kuenziwa na kutumiwa katika matangazo mengi ya biashara hususani yale yanayowalenga wananchi wa kawaida na ambao ndio wengi. Tukitazama hali ilivyo nchini Kenya kama mfano tunaona kuwa kulingana na takwimu za shughuli za kuhesabu watu (2009), Wakenya wengi husikiliza Kiswahili mara nyingi kuliko wale wanaosikiliza redio za lugha ya Kiingereza. Kutokana na mwamko huu, wafanyibiashara hutumia Kiswahili kupitia kwa matangazo anuwai ya biashara ili kuwafikia wateja wengi ambao huelewa lugha hii kwa urahisi kuliko Kiingereza ili kuongeza mauzo yao. Kwa upande mwingine stesheni husika hujipatia mapato makubwa kutokana na mauzo ya jumbe za biashara.

Matangazo ya biashara huweza pia kuwasilishwa kwa simu tamba. Wafanyibiashara wengi wamegundua umuhimu wa kutumia teknolojia ya mawasiliano katika kuwafikia wateja wengi. Matangazo ya aina hii hutayarishwa kwa kuzingatia masharti mbalimbali kama vile uonekaji mzuri kwenye simu inayohusika. Waandalizi wa jumbe hizi huhitaji makini ya hali ya juu hasa katika kuweka wazi tovuti ya shirika la biashara linalotoa tangazo hilo. Aidha, matarajio ya mtumiaji wa simu tamba, huzingatiwa kikamilifu. Kutokana na kueleweka kwa lugha ya Kiswahili miongoni mwa wananchi wengi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni wazi kuwa matangazo mengi yatatumia lugha hii kwa lengo la kupanua soko la bidhaa na huduma husika. Matokeo ya hali hii ni kuwepo kwa mauzo mengi na hivyo wahusika kupata faida kubwa.

## Kiswahili na Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani

Viwanda ni sehemu muhimu ya uchumi wa nchi. Katika juhudi za kuzalisha bidhaa viwandani, wawekezaji hutumia rasilimali watu kama njia kuu ya kuelekeza uzalishaji husika. Hapa panahitajika chombo cha mawasiliano kinachoeleweka kwa wahusika wanaofanya kazi humo ili kufanikisha shughuli nzima. Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, lugha ya Kiswahili inaweza kutekeleza jukumu kubwa katika mazingira haya. Mijadala na maelekezo anuwai muhimu viwandani yanapotekelezwa kwa lugha inayoeleweka inakuwa rahisi kufikia malengo ya uzalishaji ya makampuni husika. Hivyo ni wazi kuwa makampuni ya kibiashara yanayohusika na uzalishaji wa bidhaa yanatarajiwa kufanya juhudi za kimakusudi katika kuwashirikisha wafanyikazi wao katika mchakato wa uzalishaji kupitia kwa lugha wanayoielewa. Hili likitokea, itakuwa rahisi kuimarisha uzalishaji na hivyo kuongeza faida kutokana na mauzo ya bidhaa zitakazozalishwa.

Hatua inayofuata uzalishaji ni kuweka maelekezo ya matumizi ya bidhaa hizo mbalimbali. Haya maelekezo yana umuhimu wa kipekee kwa sababu hutoa

ujumbe kwa mtumiaji wa bidhaa hiyo ili kuepuka athari hasi kwake na kwa jamii inayoinunua. Tunasisitiza kwamba ili kutimiza lengo hili la kupasha habari, lugha inayoeleweka kwa watumiaji sharti itumike. Katika mazingira ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, lugha ya Kiswahili itafaa sana kutoa maelekezo hayo kutokana na kueleweka kwake kwa watu wengi katika eneo hili. Hata wakati kampuni za uzalishaji wa bidhaa zina mazoea ya kutoa maelekezo kwa lugha nyinginezo hususani Kiingereza, itakuwa muhimu kutoa tafsiri ya Kiswahili ili watumiaji wengi wa bidhaa hizo ambao wanaielewa lugha hiyo kunufaika. Juhudi hizi zitaimarisha mauzo ya bidhaa hizo kwa kuwa wateja watakuwa wanaelewa ni nini hicho watakuwa wananunua na namna ya kukitumia. Ikumbukwe kwamba ni hatari kununua na kutumia bidhaa ambazo mteja haelewi maelekezo kuhusu matumizi yake. Hatari hii huweza kumlenga mnunuzi na mtumiaji binafsi au jamii inayomzunguka kwa jumla.

Maelekezo ya kijumla kuhusu matumizi ya sehemu na hata vifaa mbalimbali yanastahili kutolewa kwa lugha inayoeleweka kwa wafanyikazi katika viwanda wanamofanya kazi. Kutokuwapo kwa maelekezo ya aina hii kutapelekea sehemu na vifaa husika kuhatarisha maisha ya wafanyikazi katika viwanda hivyo. Hali hii inaweza kuepukwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwa maelekezo yatatolewa kwa lugha ya Kiswahili kwa kuwa ndiyo inayoeleweka kwa watu wengi kutokana na nafasi yake kama lugha ya matumizi mapana katika eneo zima. Katika kufanya hivi, mazingira ya utendakazi yataboreshwa na hivyo kuongeza uzalishaji wa bidhaa viwandani. Matokeo ya hali hii ni kustawi kwa uchumi wa nchi husika.

Pia, ni muhimu kutaja hapa kuwa majina ya bidhaa zinazozalishwa katika viwanda vinavyopatikana katika eneo la Jumuiya ya Afrika Mashariki, yanastahili kuwa ya Kiswahili. Baadhi ya bidhaa zinazozalishwa nchini Kenya zimepewa majina ya Kiswahili kama vile unga (Jogoo, Jimbi, Soko, Pembe n.k) na mbolea (Mea na chapa Meli). Majina ya bidhaa yana athari kubwa katika kuongezeka kwa wateja wanaovutiwa hasa ikiwa wanayaelewa na wangependa kunasibishwa nayo. Ikumbukwe kwamba bidhaa nyingi zinazotengenezwa katika viwanda vya nchi mbalimbali za jumuiya, huuziwa wanunuzi katika eneo husika. Wanunuzi wengine katika nchi mbalimbali za kiafrika wanatarajiwa kuvutiwa na majina ya aina hii hasa ikiwa nchi husika zinatumia Kiswahili kama lugha mojawapo ya njia za mawasiliano ya kila siku. Katika utafiti uliofanywa kuhusu mvuto wa bidhaa kule Catalonia na Quebec, iligunduliwa kuwa raia wa maeneo hayo walipendelea bidhaa ambazo zilikuwa na majina ya lugha zao. Matokeo ya utafiti huu yanashadidia umuhimu wa kutumia lugha ya Kiswahili katika kutaja na kutoa maelezo kuhusu bidhaa zinazotengenezwa katika eneo la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ni kutokana na uzalendo wa wananchi ambapo bidhaa kama hizo zinatarajiwa kununuliwa kwa wingi na hivyo kupelekea ukuaji wa kiuchumi.

**Kiswahili na Utoaji wa Huduma**

Tunazo huduma mbalimbali ambazo huchangia ukuaji wa uchumi. Tukichukua mfano wa huduma za benki tunagundua kuwa uchumi wa nchi huzitegemea katika kuafikia ustawi wa kiuchumi. Kwa kawaida wananchi hutegemea huduma hizo wanapohitaji mikopo ya kuendeleza biashara zao na hata wakati mwingine wanapoweka akiba zao. Hii sekta huendeshwa kwa kutumia lugha inayoeleweka kwa wateja wao. Katika mazingira ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kiswahili ndiyo lugha inayotumiwa na wanajamii wengi. Hivyo katika juhudi za kuwafikia wateja wao, wasimamizi wa benki mbalimbali wanastahili kuweka mikakati ya kuboresha matumizi ya Kiswahili katika kutangaza na hata kutoa huduma mbalimbali. Ni wazi kuwa watu huvutiwa na kushawishiwa zaidi pale wanapowasilishiwa habari kwa lugha wanayoielewa vizuri. Ikumbukwe kuwa hivi sasa huduma za benki zinapatikana hata vijijini ambapo watu wengi ni watumiaji wa Kiswahili kinyume na ilivyokuwa awali ambapo huduma hizi zilijikita mijini na kuwalenga waliosoma.

Huduma nyingine ni ile ya sekta ya utalii. Uchumi wa nchi nyingi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki hutegemea mapato kutokana na utalii katika kujiendeleza. Ingawa kwa miaka mingi nchi hizi zimekuwa zikitegemea watalii kutoka nchi za kigeni, hivi sasa tunao watalii wa ndani ambao huchangia ukuaji wa sekta hii. Wizara za utalii zinapaswa kujitahidi kutoa huduma zao mbugani na hata hotelini kwa lugha ya Kiswahili ili kurahisisha mawasiliano. Juhudi za kuwafundisha watalii wa kigeni Kiswahili kupitia mipango kama vile 'ufundishaji Kiswahili kwa wageni' zinastahili kupewa kipaumbele katika nchi husika. Mpango huu umenawiri kwa kiasi kikubwa nchini Tanzania na wastahili kuigwa na nchi nyingine za eneo hili ili kuongeza mapato yanayopatikana kutoka kwa huduma hii.

**Kiswahili na Kilimo**

Kilimo ni kati ya sekta ambazo zinatarajiwa kuimarishwa ili kupelekea ukuaji wa kiuchumi. Kama njia ya kuwashirikisha wadau wote katika sekta hii, serikali za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinapaswa kutoa maelekezo na maelezo kwa lugha inayoeleweka kwa wananchi wengi. Mikutano, semina na warsha kuhusu kilimo bora zinazoandaliwa katika sehemu mbalimbali katika jumuiya ili kuwahamasisha wakulima, ziendeshwe kwa Kiswahili. Lugha ya Kiswahili itafaa sana kama msimbo wa mawasiliano katika shughuli hii nzima kutokana na kueleweka kwake na jamii pana ya eneo zima la jumuiya. Aidha, maelekezo yanayotolewa kwenye mbegu, dawa na vifaa vya kilimo, yaandikwe kwa Kiswahili na Kiingereza. Hatua hii itahakikisha kuwa dosari zinazofanywa kutokana na kutoeleweka kwa maelekezo, zinaepukwa. Kwa kufanya hivyo, umma utashirikishwa katika uzalishaji wa mazao mbalimbali ya kilimo kwa kuzingatia viwango vya ubora vilivyowekwa.

Kwa upande mwingine, maafisa wa kilimo nyanjani wanapaswa kutoa mafunzo kwa lugha zinazoeleweka kwa umma. Ifahamike kwamba maafisa wa kilimo mara nyingi hufunzwa kwa lugha ya Kiingereza wanapokuwa chuoni. Mawazo mapevu ya kiteknolojia na masuala ya kinadharia wanayofunzwa chuoni, huhitaji msimbo unaoeleweka ili kuufikia umma nyanjani. Katika jumuiya, matumizi ya lugha za kienyeji na Kiswahili, yakihimizwa, umma utapokea ujumbe unaowasilishwa kwa urahisi. Akieleza kuhusu umuhimu wa lugha za kienyeji, Bruthiaux (2002), anasema kuwa lugha hizo humwezesha mtu kufahamu uwezo wake wa kiuchumi. Pia, anaeleza kuwa ikiwa lugha husika ina mfumo wa kimaandishi, itafaa sana katika uwasilishaji wa mawazo kuhusu uchumi na uzalishaji wa mazao anuwai. Matokeo ya hali hii ni kuboreshwa kwa kilimo kule mashinani. Maeneo yenye rutuba na mvua ya kutosha katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, yatatumika inavyostahili katika ukuzaji wa mimea na hata ufugaji wa mifugo huku wakulima husika wakishirikishwa kwa matumizi ya lugha wanayoilewa.

## Hitimisho

Katika makala haya tumetalii nafasi ya Kiswahili katika ukuaji wa uchumi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tumeonyesha namna Kiswahili kinavyotumiwa kama lugha ya matumizi mapana katika eneo hili kwa lengo la kuimarisha hali ya kiuchumi. Umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika mawasiliano ya kibiashara umewekwa wazi huku ikisisitizwa kwamba lugha hii ina mchango mkubwa katika shughuli za moja kwa moja za wauzaji wa bidhaa anuwai na wateja wao. Kueleweka kwa Kiswahili miongoni mwa wananchi wa nchi husika kunakifanya kuwa chombo muhimu cha kuhamishia fikra na hisia za wahusika mbalimbali katika biashara na hatimaye kuleta ufanisi katika shughuli nzima. Aidha, umuhimu wa Kiswahili katika matangazo ya biashara umejadiliwa. Imejitokeza kwamba wawekezaji katika sekta mbalimbali za kiuchumi hupendelea kutangaza bidhaa na huduma zao kupitia kwa lugha inayoeleweka na wengi kwa kuwa wanalenga faida kubwa. Vyombo vya habari hutoa matangazo ya biashara kwa Kiswahili ili kuifikia hadhira pana na kwa faida kubwa kupitia ununuaji wa bidhaa husika. Matumizi ya Kiswahili viwandani na katika sekta mbalimbali za kutoa huduma yamejadiliwa kwa kina. Mwishoni tumependekeza kuhusu mambo yanayohitaji kufanywa na Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ili kuboresha matumizi ya Kiswahili kwa manufaa ya kiuchumi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

## Marejeleo

Bruthiaux, P. (2002). Hold your Courses: Language Education, Language Choice, and Economic Development. *TESOL Quarterly, 36, 275 – 96.*

Chiraghdin, S. na Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili.* Nairobi: Oxford University Press.

Djite, P. G. (2009). The Sociolinguistics of Development in Africa. In *African Journal of Educational Development 29, 73 – 79*

Kitula, K. (1999). *Language Development Research in 21st Century 3 (3) 3.* [online] URL:http://web.africa.ufl.edu/asq/v3/v3i3a3.htm

Mukuthuria, M. (2006). Kiswahili and its Expanding Roles of Development in East African Cooperation: A case of Uganda. *Nordic Journal of African Studies 15 (2): 154 - 165*

Nwadike, E. (2004). The Role of Igbo in Enhancing National Unity, in Oyowele (ed) *Nigerian Languages for National Development and Unity.* Ibadan: Longman Communication.

Prah, K. (1993). *Mother-Tongue for Scientific and Technological Development in Africa.* German Education for International Development.

TUKI (2009). *English-Swahili Dictionary (3rd Edition).* Dar es Salaam: TUKI.